JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI
BODI YA MAJI UROKI-BOMANG 'OMBE,
S. L. P 200,
HAI

PICHA

FOMU YA MAOMBI PAMOJA NA MKATABA WA KUUNGANISHA MAJI

1.0 HABARI ZA MWOMBAJI **PA Book: ……**

1.1 Jina la Mwombaji: .....

1.2 Kijiji/ Mtaa: ..... Kitalu: Namba: .....

1.3 Kata: ..... Chanzo: .....

1.4 Anwani ya Posta: .....

1.5 Simu: .....

1.6 Nakala ya Kitambulisho cha **NIDA** au **Leseni ya Udereva** na NAMBA pia.

NIDA ☐☐☐☐☐☐☐☐-☐☐☐☐☐-☐☐☐☐☐-☐☐

LESENI YA UDEREVA ☐☐☐☐☐☐☐☐☐☐

2.0 MAOMBI

2.1 Mimi mtajwa hapo juu natuma maombi yangu kwa Bodi ya Maji Uroki-Bomang'ombe na iwapo Bodi itakubali maombi haya nitaunganishiwa maji baada ya kukamilisha taratibu zote.

Bodi haitalazimishwa / kuhusishwa na lolote katika kukubali maombi haya.

3.0 TARATIBU

3.1 Taratibu zote za Mipango Miji, matumizi ya ardhi, pamoja na haki zote husika zitapaswa zikamilishwe nami kabla ya Bodi kuunganisha bomba la maji ninaloomba.

3.2 Kadhalika Bodi itaunganisha bomba hilo pale tu ambapo nitasaini fomu ya maombi haya na kukubaliwa na Bodi.

3.3 Mimi mwombaji ndiye mwenye jukumu la kuhakikisha njia ya mtaro wa bomba litakalounganishwa unapita wapi, na pia nihakikishe kwamba nimeshapata vibali vya watu na mamlaka zote zinazohusika. Nitahakikisha pia kwamba mipaka ya ardhi yangu ni sahihi na kwamba nitabeba jukumu lote la madai na gharama ambazo Bodi itadaiwa iwapo habari nilizotoa kwa Bodi kuhusu njia ya mtaro na mipaka ya ardhi yangu sio sahihi.

4.0 GHARAMA ZA BOMBA NA VIUNGO

4.1 Nitagharamia ununuzi wa bomba na viungio vyote ambavyo vitahitajika kuwawezesha mafundi wa Bodi kuunganisha bomba ninaloliomba.

4.2 Nitanunua bomba na vifaa vya maunganisho vyote kutoka ofisi ya Bodi ya Maji Uroki-Bomang'ombe.

4.3 Nitagharimia uchimbaji wa mtaro wa bomba lililotajwa pamoja na njia iliyokubaliwa kufuatana na maelekezo ya mafundi wa Bodi.

4.4 Iwapo njia ya bomba inakata barabara, basi litakuwa jukumu langu kupata kibali cha kuchimba mtaro kukata barabara hiyo. Kadhalika nitagharimia kuweka bomba maalum la kuzuia mkandamizo wa magari juu ya bomba litakalounganishwa.

5.0 UMILIKAJI WA BOMBA

5.1 Nakiri kwamba mabomba yote yaliyogharamiwa na Bodi ni mali ya Bodi.

5.2 Nakiri pia kwamba bomba, mita na viungio vyote nilivyogharamia ili Bodi iweze kuunganisha bomba nililoliomba vitakuwa mali ya Bodi mara tu vitu hivyo vitakapofungwa kwenye bomba kuu. Sintokuwa kikwazo kumzuia mteja mwingine kuunganishiwa maji toka bomba hili.

5.3 Sehemu ya bomba na dira inayonihusu itakuwa chini ya uangalizi wangu. Uharibifu wowote utakaotokea kwenye sehemu ya bomba baada ya mita pamoja na dira inayonihusu ni jukumu langu na marekebisho au matengenezo yoyote kwenye sehemu hiyo ni juu yangu mimi mwenyewe. Hata hivyo, nitakubali ushauri wowote wa mafundi wa Bodi kuhusu matengenezo ya sehemu hiyo ya bomba.

6.0 VIWANGO VYA MALIPO NA ANKARA

6.1 Nakiri kwamba RUWASA ndiyo yenye mamlaka yote ya kuweka ada ya kulipia maji, na ninaahidi kulipia ankara kabla ya siku saba (7) baada ya ankara ya mwezi kutoka. Nikichelewa niko tayari kulipa ankara yote pamoja na kiwango kilichowekwa na Bodi kama faini ***(Tshs. 20,000/=)***. Pia sitolalamika popote endapo maji yakikatwa kwa kuchelewesha kulipa ankara zangu za maji.

6.2 Hali kadhalika, Bodi itakuwa na haki na mamlaka ya kukata maji iwapo zitapita siku saba (7) tangu Bodi kutoa taarifa kwangu kuhusu kipengele chochote cha Mkataba huu ambacho nitakuwa nimekivunja, na iwapo katika siku hizo saba(7) nitakuwa sijachukua hatua zozote za kutatua au kusuluhisha tatizo nililotaarifiwa.

6.3 Naahidi kwamba sitaiba maji kinyume na utaratibu. Endapo nitagundulika kuharibu dira, kuharibu/kushiriki kusaidia kuharibu miundombinu ya maji ya **BODI** au kuiba maji, Bodi itanikatia huduma na kutozwa faini kwa mujibu wa ***SHERIA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA NAMBA 5 YA MWAKA 2019***. Kama sitalipa nitapelekwa katika vyombo vya sheria na kukosa huduma ya maji kabisa. Si lazima Bodi ikubali ombi langu la msamaha.

7.0 MENGINEYO

Pande zote katika Mkataba huu, yaani mimi mwombaji pamoja na Bodi tutatumia kila jitihada kuhakikisha kuwa Mkataba huu, baada ya kukubaliwa na kusainiwa na Bodi, unatekelezwa. Iwapo Mwombaji atakuwa na malalamiko yoyote, hatakuwa na haki ya kuchukua hatua yoyote ya kisheria kabla hajawasiliana na Bodi na kabla jitihada za pamoja za kutatua tatizo

lililoleta malalamiko hazijashindwa. Mteja akikiuka taratibu za matumizi ya maji atakuwa amevunja mkataba huu na atasitishiwa huduma ya maji mara moja.

SAHIHI YA MWOMBAJI .....

TAREHE: .....

Wadhamini wa Mwombaji

Ninamfahamu mwombaji na naahidi kwamba atalipia ankara zake bila matatizo yoyote na ikiwa atashindwa kulipa, basi mimi nitawajibika kulipa gharama zote mara moja.

	JINA	WADHIFA	SAINI	TAREHE
1.	.....			
2.	.....			

Eneo langu limekaguliwa na kuonekana liko sawa pamoja na mipaka yote ni sahihi. Pia mtaro utapita eneo lisilo na mgogoro.

Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa **Jina**: ..... **Saini:** .....

Mjumbe wa Kamati ya Maji **Jina**: ..... **Saini**: .....

Taarifa fupi ya Mjumbe wa K/maji **Simu**:..... Umbali wa Mtaro **Mita**:……

KIBALI CHA BODI

Bodi ya Maji Uroki-Bomang'ombe, baada ya kupokea na kupitia maombi yaliyoletwa na mwombaji kama yanavyoonekana hapo juu **IMEKUBALI / IMEKATAA** maombi hayo na kufanya vipengele vyote vinavyoonekana hapo juu kuwa na uthabiti wa kisheria.

Leo tarehe: ..... Mwezi: ..... Mwaka: .....

Katibu wa Bodi Jina:..... Saini .....

<u>ANGALIZO:</u> MAJI NI KWA AJILI YA MATUMIZI ULIYO OMBEA. KINYUME CHAKE UTASITISHIWA HUDUMA KWA GHARAMA ZAKO!

BODI YA MAJI UROKI – BOMANG'OMBE.

KWA: BW / BIBI / BI .....

YAH: OMBI LAKO LA KUUNGANISHIWA MAJI KATIKA MAKAZI:

Tafadhali rejea maelezo yako katika fomu zilizotangulia kama ulivyojaza

Fundi wetu amepima eneo lako na kupata umbali wa mita ..... Fundi: _____

Matumizi ya maji yatakua kwa ajili ya ***Makazi/Taasisi/Biashara*** .....

Jumla ya vifaa kamili vinavyohitajika kukupatia huduma hii ni kama ilivyoorodheshwa hapa chini:-

NA.	JINA LA KIFAA	KIPIMO	KIASI
1			
2			
3			
4			
5			
6			
7			
8			
9			
10			
11			
12			
13			
14			
15			
16			
17			
18			
19			

(V) MTEJA ATANUNUA VIFAA VYOTE VYA MAUNGANISHO KWENYE BODI.
(X) MALIPO YOTE YATAFANYIKA KWA KUTUMIA KUMBUKUMBU NAMBA(CONTROL NUMBER) NA SIO KWA NJIA NYINGINE YEYOTE.
ANGALIZO: MALIPO YATAKAYOFANYIKA KWA NJIA TOFAUTI NA KUMBUKUMBU NAMBA (CONTROL NUMBER) ILIYOTOLEWA NA OFISI HAYATOTAMBULIKA NA BODI.

KWA MATUMIZI YA OFISI TU;

Jumla ya gharama zote za maunganisho mteja anazotakiwa kulipa kiasi cha **Tshs**. .....

AHUDUMIWE / ASIHUDUMIWE

……..	……..	……
Meneja / Fundi Mkuu	**Fundi wa Bodi**	**Mhasibu Mkuu**

MUHIMU:
MTEJA ANAHITAJIKA KUJENGA CHEMBA MWENYEWE NAKUWEKA MFUNIKO IMARA (TOFALI 12, SEMENTI ½ MFUKO, KOKOTO, MFUNIKO WA 50cm-50cm & MCHANGA WA KUJENGEA BOKSI LA MITA) sababu mita ikipasuliwa Gharam ani juu ya Mteja ambaye hajajenga chemba kwa wakati.

MKATABA WA KUUNGANISHA MAJI

BODI YA MAJI UROKI – BOMANG'OMBE.

KWA MATUMIZI YA OFISI TU:

(IJAZWE NA FUNDI WA BODI ALIYEPIMA ENEO LA MWOMBAJI) **FUNDI: ……**

JINA LA MWOMBAJI: ..... **Kijiji:** .....

KITALU: …… NAMBA YA Kiwanja: ……..

Mwombaji ataunganishiwa kutoka tawi la.....

Ukubwa wa Bomba ni ..... Aina ya Bomba: .....

Urefu wa Bomba: .....

Tariff……

Chemba ya mita itahitajika? **NDIYO / HAPANA**

OMBI HILI **LIMEKUBALIWA / HALIKUKUBALIWA**

SABABU:

RAMANI:

IMEUNGANISHWA NA: ..... **TAREHE:** ..... **SAINI** .....

IMEKAGULIWA NA: ..... **TAREHE** ..... **SAINI** .....

BODI YA MAJI UROKI – BOMANG'OMBE.

UTARATIBU WA KUANDAA ANKARA ZA MAJI NA UKUSANYAJI WA MALIPO

- Mhudumu wa bomba (Pipeline Attendant) wa kila Kijiji/Mtaa hutembelea wateja wote wa eneo husika; ili kusoma Dira zao na kurekodi katika simu maalumu.

- Mhudumu wa bomba humpelekea Meneja/Mhasibu simu hiyo maalumu kwa ajili ya kutengeneza ankara (bili).

- Ankara hutengenezwa na kutumwa kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) kwa kila mteja, ujumbe mfupi (SMS) huo utaambatanishwa pamoja na namba ya malipo (Control Number) ambayo mteja ataitumia kufanya malipo ya ankara ya maji za kila mwezi na italipwa ndani ya siku 7.

- Kwa wale wakala (Agents) ambao hupokea malipo ya maji kwenye vilula (PT - Public Taps) watakapokamilisha malipo yao ya ankara kwa kupitia namba ya malipo (control number), Mhasibu atamlipa wakala asilimia iliyoainishwa ya makusanyo hayo kama kichocheo (incentive) kwa utaratibu ofisi umeuweka.

- Wateja wenye matawi binafsi ya nyumbani wanapaswa kulipia ankara (bili) zao ndani ya siku saba tangu mwezi wa Ankara kupita, vinginevyo itabidi mteja asitishiwe huduma ya maji na atarudishwa pale atakapokuwa amemaliza kulipa ankara yake yote pamoja na faini ya shilingi 20,000/=. Endapo mteja hatolipa kabisa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mimi ..... nimesoma, nimeelewa na ninakubali.

Sahihi: ..... Tarehe: .....

Imeamuliwa na:

BODI YA MAJI UROKI – BOMANG'OMBE.